

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME



TANGAZO LA ZABUNI NA LGA/049/NC/G/C/2017/2018

TAREHE 12/5/2017

Halmashauri ya Wilaya ya Same inatoa tangazo la zabuni (PreQualification) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya utoaji huduma mbalimbali na uuzaaji bidhaa mbalimbali. Tangazo hili la zabuni liko wazi kwa kampuni, taasisi yoyote iliyosajiliwa kisheria kufanya biashara au kutoa huduma inayohusiana na shughuli/huduma zilizotangazwa hapa chini.

KUNDI	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI
1	Huduma ya unyonyaji maji taka Halmashauri ya (W) Same	LGA/O49/NC/2017/2018/01
2	Huduma ya Uchapishaji wa nyaraka mabalimbali (Printing)	LGA/O49/NC/2017/2018/02
3	Huduma ya mapambo katika sherehe mbalimabali za serikali.	LGA/O49/NC/2017/2018/03
4	Upangishaji wa Mgahawa uliopo Makao Makuu ya Halmashauri (W) Same	LGA/O49/ NC/2017/2018/04
5	Upangishaji wa Baa ya PADECO (Iliyopo stendi kuu ya Mabasi Same)	LGA/O49/ NC/2017/2018/05
6	Huduma ya Matengenezo, Vifaa Tiba na Mashine za Hospitali.	LGA/O49/ NC/2017/2018/06
7	Uuzaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo	LGA/O49/G/2017/2018/01
8	Uzaji wa Gesi Tiba (Medical gas)	LGA/O49/G/2017/2018/02
9	Uuzaji wa Dawa / Vifaa Tiba (Hospital Equipments) na vifaa vya Maabara	LGA/O49/G/2017/2018/03

SIFA NA MASHARTI KWA WAOMBAJI WOTE:

- 1) Mwombaji ni lazima ataje bei ya huduma atakayotoa kwa Halmashauri (Price list). Isipokuwa zabuni ya matengenezo na upambaji
- 2) Mwombaji aambatanishe hati ya usajili “Extract Register” au “Memorandum of Association” picha za wakurugenzi/wamiliki iwapo mwombaji ni kampuni, kikundi au ushirika.
- 3) Mwombaji binafsi aambatanishe picha yake katika Maombi na igongwe muhuri wa mtendaji kata/kijiji.
- 4) Mwombaji aonyeshe uzoefu wake juu ya zabuni anayoomba.
- 5) Mwombaji aeleze mahali ofisi yake ilipo./namba ya nyumba.
 - a) Mwombaji wa uuzaaji wa dawa na vifaa vya hospitali awe amesajiliwa na Baraza la Pharmacy (Pharmacy council of Tanzania / TFDA na awe na mtaalam (Mfamasia) aliyesajiliwa na Baraza la (madawa).
 - b) Mwombaji wa uuzaaji wa Pembejeo za kilimo na mifugo awe na vibali vinavyomruhusu kufanya biashara hiyo kutoka TPRI/TFRA
- 6) Mwombaji awe tayari kufanya kazi/kutoa huduma kabla ya malipo.(Kwa LPO).
- 7) Ada ya maombi kwa kila kundi ni TSh. 100,000/= fedha ambazo hazitarejeshwa.
- 8) Mwombaji wa ukodishaji wa Mgahawa / Baa ya PADECO ataje kiasi atakacholipa kwa mwezi (kodi ya pango)
- 9) Mwombaji wa ukodishaji wa Mgahawa / Baa ya PADECO atalazimika kulipa kodi ya pango ya muda wa miezi mitatu (Dhamana ya utendaji kazi) kabla ya kuanza kazi

Namna ya kutuma maombi.

1. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha na lakiri na isionyeshe alama ye yeyote toka kwa mwombaji, na ndani ya bahasha iambatanishwe stakabadhi halisi ya malipo ya ada ya maombi na vivuli vya leseni na hati mbalimbali zenyenye kumtambulisha mwombaji.
2. Juu kabisa ya bahasha yenyenye maombi paandikwe kwa herufi kubwa UUZAJI/HUDUMA YA maombi yatumwe kwa:-

KATIBU BODI YA ZABUNI (W)

S.L.P 138,

SAME,KILIMANJARO. na kutumbukizwa kwenye sanduku la zabuni ofisi ya Mkurugenzi (W)

3. Siku ya mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **25/05/2017 saa nne (4.00)** asubuhi na ufunguzi wa zabuni hizo utafanyika kuanzia saa **4.00** katika ukumbi wa Halmashauri ya Same.

4. Maombi yatakayochelewa au yaliyotumwa kwa fax, telex au telegram hayatafikiriwa.
5. Bodi ya zabuni hailazimiki kukubali zabuni ya juu au ya chini.

ANNA - CLAIRE -SHIJA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SAME.

Tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya wilaya ya Same na mbao za matangazo Halmashauri ya wilaya Same(www.samedc.go.tz)